**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA ELIMU YA AMALI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

**Machi, 2025**

MZUMBE BOOK PROJECT

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................ iii

SHUKURANI ........................................................ v

VIFUPISHO ........................................................ vii

MAANA YA MANENO ........................................................ viii

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

1.1 Usuli ........................................................ 1

1.2 Malengo ya Mwongozo ........................................................ 7

1.2.2 Malengo Mahususi ........................................................ 7

1.3 Umuhimu wa Mwongozo ........................................................ 8

1.4 Walengwa wa Mwongozo ........................................................ 9

1.5 Mawanda ya Mwongozo ........................................................ 9

2.0 UTEKELEZAJI WA UTOAJI WA MAFUNZO YA ELIMU YA AMALI ........................................................ 11

2.1 Maeneo Stahiki katika Utekelezaji wa Mafunzo ya Elimu ya Amali ........................................................ 12

2..2 Maelekezo ya Utekelezaji wa Elimu ya Amali ............. 17

3.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU ........................ 23

4.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ........................................................ 42

4.1 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini ........................................................ 42

4.2 Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Ngazi Mbalimbali ........................................................ 43


MZUMBE BOOK PROJECT

4.2.1 Ngazi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) .......... 43
4.2.2 Ngazi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) .......... 44
4.2.3 Ngazi ya Mkoa .......... 45
4.2.4 Ngazi ya Halmashauri .......... 45
4.2.5 Ngazi ya Shule .......... 46
4.3 Viashiria vya Mafanikio ya Elimu ya Amali .......... 46
MAREJELEO .......... 48
VIAMBATISHO .......... 52

MZUMBE BOOK PROJECT

# DIBAJI

Dira ya Elimu na Mafunzo nchini ni kumjenga Mtanzania mwenye ujuzi, maarifa, na mtazamo chanya, ili aweze kuchangia maendeleo ya Taifa. Aidha, ili kufanikisha dira hii, ni muhimu kuweka mifumo na taratibu madhubuti zitakazochochea ari ya kujifunza kwa Watanzania, na hivyo kuwezesha kufanikisha malengo yao binafsi na ya Taifa kwa ujumla.

Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imejizatiti kuinua uchumi wa nchi kwa kuhakikisha kuwa wahitimu wa elimu wanakuwa na uwezo wa kuajiriwa au kujiajiri. Mafanikio haya hayawezi kupatikana bila maboresho ya Sera na Mitaala, kutokana na changamoto zilizokuwepo ambazo zilikwamisha matokeo bora ya ujifunzaji. Miongoni mwa changamoto hizo ni udhaifu katika mfumo na muundo wa elimu, ambao ulitoa mafunzo kwa jumla bila kuzingatia mahitaji halisi ya soko la ajira na mazingira ya kujifunzia.

Kutokana na changamoto hizo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imefanya marekebisho katika

MZUMBE BOOK PROJECT

Sera ya Elimu na Mitaala kwa lengo la kuboresha mfumo wa elimu nchini. Mojawapo ya maboresho haya ni kuingizwa kwa Elimu ya Amali katika shule, hatua inayolenga kuhakikisha kuwa wahitimu wanapata maarifa na ujuzi wa kazi unaowezesha kujitegemea.

Kwa muktadha huo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Amali katika Shule za Sekondari ili kuhakikisha kuwa elimu hii inatekelezwa kwa ufanisi. Mwongozo huu utakuwa nyenzo muhimu kwa watekelezaji na wasimamizi wa elimu ili kuhakikisha kuwa kila mdau anatekeleza wajibu wake ipasavyo kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa.

Ni matumaini yangu kuwa Mwongozo huu utatumika ipasavyo katika kufanikisha lengo la kuwaandaa vijana wa Kitanzania kwa maisha yenye tija na mchango chanya kwa Taifa.

MZUMBE BOOK PROJECT

Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

## SHUKURANI

Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Amali katika Shule za Sekondari nchini Tanzania umeandaliwa kwa ushirikiano wa wataalamu na wadau mbalimbali. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu kutoka wizara na taasisi mbalimbali waliotoa mchango wao muhimu katika maandalizi ya mwongozo huu.

Tunapenda kutoa pongezi na shukurani maalumu kwa taasisi na wizara zilizoshiriki katika kazi hii muhimu, zikiwemo: Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( OR-TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Sheria na Katiba, Wizara ya Habari, Masiliano na Teknolojia ya Habari, pamoja na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Vilevile, tunashukuru kwa dhati wadau wengine wote waliotoa mchango wao katika hatua mbalimbali za maandalizi ya mwongozo huu.

Shukurani za pekee zinatolewa kwa maafisa wa WyEST na OR – TAMISEMI kwa mchango wao mkubwa katika

MZUMBE BOOK PROJECT

kuratibu na kuongoza jopo la wataalamu wa fani mbalimbali tangu hatua za awali za uandaaji hadi kukamilika kwa mwongozo huu.

Kwa pamoja, tumeweza kuweka msingi imara wa kuhakikisha kuwa Elimu ya Amali inatekelezwa kwa ufanisi katika shule za sekondari, ili kuwajengea wanafunzi maarifa, ujuzi na stadi zinazowezesha kujitegemea na kuchangia maendeleo ya Taifa.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**KAMISHANA WA ELIMU**

MZUMBE BOOK PROJECT

VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADEM | Agency for the Development of Education Management |
| CTE | Career and Technical Education |
| NACTVET | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| NECTA | Baraza la Mitihani la Tanzania |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Masiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TVET | Technical and Vocational Education and Training |
| VETA | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

MZUMBE BOOK PROJECT

## MAANA YA MANENO

| | |
|---|---|
| **Elimu ya Amali** | Elimu ya maarifa na ujuzi wa kazi. |
| **Ujuzi wa Kazi** | Maarifa na stadi zinazomwezesha mtu kufanya kazi fulani kwa ufanisi. |
| **Ujasiriamali** | Uwezo wa kubuni na kuendeleza biashara au shughuli za kiuchumi kwa lengo la kupata faida. |
| **Sekta Binafsi** | Mashirika na makampuni yasiyo ya Serikali yanayoshiriki katika utoaji wa huduma na uzalishaji wa bidhaa. |
| **Mitihani ya Vitendo** | Upimaji wa wanafunzi unaolenga kupima ujuzi wao kwa njia ya vitendo badala ya maswali ya nadharia. |

MZUMBE BOOK PROJECT

| | |
|---|---|
| ***Apprenticeship*** | Mfumo wa mafunzo ambapo mwanafunzi anapata ujuzi wa kazi kwa kufanya kazi chini ya usimamizi wa mtaalamu. |
| ***Dual Vocational Training*** | Mfumo wa elimu unaochanganya mafunzo ya darasani na mafunzo ya vitendo kazini ili kuongeza ufanisi wa wanafunzi. |
| **Mafunzo kwa Vitendo** | Mazoezi ya kazi yanayomwezesha mwanafunzi kutumia maarifa aliyojifunza kwa vitendo. |

MZUMBE BOOK PROJECT.

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Elimu ya Amali inalenga kuwezesha wanafunzi wa ngazi zote kupata maarifa, ujuzi, umahiri na stadi za ujasiriamali ili kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. Elimu hii inatekelezwa kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023), ambayo inalenga kuimarisha upatikanaji wa ujuzi wa kazi na kujiajiri kwa wahitimu kwa kuunganisha mafunzo ya nadharia na vitendo.

Pamoja na hayo, inawapatia wanafunzi fursa ya kujifunza kwa vitendo katika sekta mbalimbali za uzalishaji kama vile viwandani, mashambani, uvuvi na utoaji wa huduma. Kutokana na hayo, Elimu ya Amali inahakikisha kuwa wahitimu wanakuwa na ujuzi unaowezesha kujiajiri au kuajiriwa kwa ufanisi kulingana na mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya teknolojia.

Katika ngazi ya kimataifa, juhudi za kuimarisha Elimu ya Amali zinaonekana katika nchi mbalimbali za Ulaya, Amerika, Asia, na Afrika. Mifumo hii imeathiri kwa kiasi

MZUMBE BOOK PROJECT

kikubwa maboresho ya Elimu ya Amali nchini Tanzania kwa kutoa mifano bora ya utekelezaji wa mafunzo ya ufundi na ushirikiano na sekta binafsi. Kwa mfano, mageuzi katika mitaala ya Elimu ya Amali nchini Tanzania yanafanana na mfumo wa *Dual Vocational Training* wa Ujerumani ambapo ujifunzaji wake unahusisha ushirikiano wa karibu kati ya viwanda na taasisi za elimu ambapo wanafunzi wanapata mafunzo ya vitendo kwa asilimia 70 na nadharia kwa asilimia 30. Mfumo huu umefanikiwa kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana na kuchangia maendeleo ya uchumi wa nchi husika (Federal Institute for Vocational Education and Training, 2021). Vilevile, Uswisi imefanikiwa kwa kutumia mfumo wa Elimu ya Amali ambapo zaidi ya asilimia 60 ya vijana wanashiriki katika programu za mafunzo ya kazi kupitia ushirikiano kati ya waajiri na taasisi za elimu, hali inayosaidia kuzalisha wahitimu wenye ujuzi wa kazi unaohitajika katika sekta mbalimbali (Swiss Federal Institute for Vocational Education and Training, 2020).

Katika bara la Amerika, mfumo wa *Career and Technical Education (CTE)* wa Marekani umefanikiwa kuwezesha wanafunzi kupata ujuzi wa vitendo kwa kushirikiana na

MZUMBE BOOK PROJECT

makampuni, sekta ya viwanda na taasisi za elimu ya juu. Mfumo huu umechangia katika kupunguza ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na kuongeza ushirikiano kati ya sekta ya elimu na soko la ajira (National Center for Education Statistics, 2021). Vilevile, nchini Kanada, mfumo wa *Apprenticeship Training* umefanikiwa kwa kutoa mafunzo ya kazi kwa wanafunzi wanaojiunga na sekta ya ujuzi wa ufundi, hatua ambayo imechangia kupunguza pengo kati ya elimu na mahitaji ya soko la ajira (Government of Canada, 2022).

Barani Asia, nchi ya Korea Kusini imeanzisha mfumo wa *Meister High Schools* kwa lengo la kutoa Elimu ya Amali yenye viwango vya juu, ambapo wanafunzi hupewa mafunzo ya kiufundi yanayoshirikisha sekta binafsi. Mfumo huu umepelekea mafanikio makubwa katika kuzalisha wahitimu wenye sifa zinazohitajika katika sekta ya viwanda na teknolojia (Lee & Lee, 2020). China nayo imefanikiwa kuboresha Elimu ya Amali kupitia mfumo wake wa *Vocational Education and Training (VET)*, ambao unahusisha mabadiliko ya mitaala ili kuendana na maendeleo ya kiteknolojia na mahitaji ya soko la ajira

MZUMBE BOOK PROJECT

(Ministry of Education of the People's Republic of China, 2021).

Katika bara la Afrika, nchi kama Afrika Kusini imefanikiwa katika kuimarisha Elimu ya Amali kupitia *Technical and Vocational Education and Training (TVET)*. Mfumo huu umeunganishwa na sekta binafsi ili kuhakikisha wahitimu wanapata mafunzo ya vitendo kupitia programu za mafunzo kazini (internship) na ushirikiano wa moja kwa moja na waajiri (Department of Higher Education and Training, 2022). Vilevile, Rwanda imeboresha mfumo wa Elimu ya Amali kwa kuanzisha VETA (Vocational Education and Training Authority) inayosimamia vyuo vya ufundi ili kuongeza idadi ya vijana wanaopata mafunzo ya ujuzi wa kazi kupitia mitandao ya mafunzo kwa vitendo.

Mifumo hii ya nchi mbalimbali imedhihirisha kuwa Elimu ya Amali inachangia kukuza uchumi, kupunguza ukosefu wa ajira na kuhakikisha kuwa wahitimu wanapata ujuzi wa vitendo unaohitajika katika soko la ajira. Tanzania inaweza kujifunza kutoka mifumo hii kwa kuboresha ushirikiano kati ya shule, vyuo vya amali, na sekta binafsi ili kuwezesha mafunzo ya vitendo yenye tija zaidi. Vilevile, uwekezaji

MZUMBE BOOK PROJECT

katika miundombinu na vifaa vya kufundishia utaongeza ufanisi wa Elimu ya Amali na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata uzoefu wa kazi unaohitajika kabla ya kuingia kwenye soko la ajira. Hata hivyo, ingawa mifumo hiyo imeonyesha mafanikio makubwa, changamoto mbalimbali bado zimeathiri utekelezaji wa Elimu ya Amali katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania.

Pamoja na jitihada za kuboresha mfumo wa elimu nchini, changamoto kadhaa zilibainika na kuhitaji mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Kwanza, kutokuwepo kwa ulinganifu kati ya mitaala na mahitaji ya soko la ajira kulisababisha wahitimu wengi kukosa ujuzi unaohitajika. Pili, upungufu wa walimu waliobobea katika fani za amali uliathiri ubora wa elimu hiyo. Zaidi ya hayo, uchache wa rasilimali muhimu za kufundishia na kujifunzia kama vile karakana, maabara na mazingira nyumbufu ya kujifunzia kwa vitendo ulifanya Elimu ya Amali kutokuwa na ufanisi uliokusudiwa. Sambamba na hayo, udhaifu wa ushirikiano kati ya taasisi za elimu na sekta ya uzalishaji ulisababisha wahitimu wengi kukosa uzoefu wa vitendo unaohitajika katika soko la ajira. Hatimaye, kukosekana

MZUMBE BOOK PROJECT

kwa mfumo thabiti wa upimaji wa Elimu ya Amali kulifanya iwe vigumu kupima ufanisi wa mitaala na mwendelezo wa wahitimu katika sekta mbalimbali.

Kwa kuzingatia changamoto hizi, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilifanya mapitio ya sera na kuja na Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 (Toleo la 2023). Tamko la Mojawapo la sera linasisitiza kuwepo kwa mitaala bora inayohusiana na mahitaji ya soko la ajira na kuweka mifumo thabiti ya ushirikiano kati ya shule, vyuo, na sekta binafsi ili kuboresha Elimu ya Amali na kuhakikisha wahitimu wanakuwa na stadi zinazowezesha kujiajiri au kuajiriwa kwa ufanisi. Hatua hii inalenga kuhakikisha Elimu ya Amali inakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa kwa kuwajengea vijana uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi.

Kwa msingi huo, Mwongozo wa Utekelezaji wa Elimu ya Amali katika Shule za Sekondari umeandaliwa ili kusaidia wadau wote wa elimu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hivyo, mwongozo huu umebainisha maeneo muhimu ya kuzingatia katika utoaji wa elimu ya Elimu ya Amali pamoja na majukumu ya wadau mbalimbali wa elimu.

MZUMBE BOOK PROJECT

Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa Elimu ya Amali inakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa kwa kuwapatia wanafunzi ujuzi wa kazi unaowezesha kuwa washindani wa kweli katika soko la ajira la ndani na kimataifa.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

### 1.2.1 Lengo Kuu

Mwongozo huu unalenga kuhakikisha kuwa Elimu ya Amali inatekelezwa kwa ufanisi ili kuandaa vijana wenye ujuzi, maarifa na stadi zinazowezesha kujiajiri na kuajiriwa kulingana na mahitaji ya soko la ajira la ndani na kimataifa.

### 1.2.2 Malengo Mahususi

Mwongozo huu una Malengo Mahususi yafuatayo:

i) Kuelekeza utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa kuzingatia mitaala iliyoboreshwa;
ii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa kujenga miundombinu na kuwezesha vifaa vya kufundishia;
iii) Kueleza majukumu ya wadau katika kusimamia na kuendeleza Elimu ya Amali;

MZUMBE BOOK PROJECT

iv) Kuhamasisha ushirikiano kati ya shule na sekta binafsi ili kuongeza fursa za mafunzo na ajira; na
v) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji na usimamiaji wa utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali katika shule za sekondari.

### 1.3 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu unatoa dira ya utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa kuoanisha mitaala na mahitaji ya soko la ajira. Unahimiza kuwa na ushirikiano kati ya wadau wa elimu na sekta binafsi kwa kuboresha miundombinu na kuongeza fursa za mafunzo kwa vitendo. Pia, unahimiza matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa utoaji wa Elimu ya Amali ili kuwajengea wanafunzi ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Mwongozo huu pia unaelekeza uwepo wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya wanafunzi na ufanisi wa utekelezaji wa mitaala ili kuimarisha ubora wa Elimu ya Amali nchini.

MZUMBE BOOK PROJECT

### 1.4 Walengwa wa Mwongozo

Walengwa na watumiaji wa mwongozo huu ni viongozi na maafisa wa Serikali waliopo katika ngazi ya WyEST, OR – TAMISEMI, Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi zake, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi, Vyombo vya habari, Wabia wa Maendeleo, Vyuo, Shule, Jamii na wazazi, walimu wa Elimu ya Amali na wanafunzi.

### 1.5 Mawanda ya Mwongozo

Mwongozo huu unashughulikia maeneo mbalimbali muhimu kwa utekelezaji wa Elimu ya Amali katika shule za sekondari, ikiwemo:

i) **Mitaala na mbinu za kufundishia** – Kubainisha muundo wa mitaala, mbinu bora za kufundishia na ujifunzaji unaozingatia vitendo.

ii) **Miundombinu na vifaa vya kujifunzia** – Kuzingatia upatikanaji wa karakana, maabara, na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia.

MZUMBE BOOK PROJECT

iii) **Ushirikiano wa wadau** – Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya elimu, serikali, sekta binafsi, na jamii katika kufanikisha Elimu ya Amali.

iv) **Mafunzo kwa vitendo** – Kuhakikisha kuwa Elimu ya Amali inajumuisha sehemu ya mafunzo kwa vitendo ili kuongeza ujuzi wa wanafunzi.

v) **Tathmini na ufuatiliaji** – Kuweka mifumo ya tathmini ya maendeleo ya wanafunzi na utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa ujumla.

MZUMBE BOOK PROJECT

## 2.0 UTEKELEZAJI WA UTOAJI WA MAFUNZO YA ELIMU YA AMALI

Serikali ya Tanzania, kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, imeweka msingi wa utekelezaji wa Elimu ya Amali ili kuimarisha ujuzi na weledi kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu. Sera hii inatamka wazi katika kifungu cha 3.1.1.7 kuwa:

*"Elimu ya sekondari ya chini, yaani kidato cha kwanza hadi cha nne, itagawanyika katika mikondo miwili: mkondo wa elimu ya jumla na mkondo wa Elimu ya Amali."*

Aidha, kifungu cha 3.1.1.9 kinaeleza kuwa:*"Elimu ya sekondari ya juu, yaani kidato cha tano na sita, au Elimu ya Amali sanifu, itakuwa hitaji la msingi kwa ajili ya kujiunga na elimu ya juu."*

Vilevile, kifungu cha 3.1.1.10 kinafafanua kuwa: *"Elimu ya juu itakuwa elimu inayofuata baada ya elimu ya sekondari na itagawanyika katika mikondo miwili: mkondo wa elimu ya jumla na mkondo wa Elimu ya Amali."*

Kwa kuzingatia maelekezo haya ya sera, Serikali imeanza rasmi utekelezaji wa Elimu ya Amali katika ngazi ya sekondari ya chini kuanzia mwaka wa masomo 2024, kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza. Hatua hii inalenga

MZUMBE BOOK PROJECT

kuwaandaa wanafunzi kupata maarifa na stadi za kazi zinazohitajika katika soko la ajira na maendeleo ya kijamii. Aidha, utekelezaji wa Elimu ya Amali utaendelea katika ngazi zinazofuata kuanzia mwaka wa masomo 2025 kwa kuzingatia utaratibu utakaokuwa unatolewa na Serikali. Ili kuhakikisha kuwa elimu hii inatekelezwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu inapaswa kuzingatia malengo mahususi yaliyoainishwa katika mwongozo huu.

### 2.1 Maeneo Stahiki katika Utekelezaji wa Mafunzo ya Elimu ya Amali

Mafunzo ya Elimu ya Amali yakitekelezwa kwa ufanisi yatawezesha wahitimu wa ngazi mbalimbali kujiunga na elimu ya juu na mafunzo ya amali sanifu baada ya elimu ya sekondari. Hatimaye, wahitimu wataweza kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia mazingira yanayowazunguka. Utekelezaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali kwa ufanisi unapaswa kuzingatia maeneo yafuatayo:

MZUMBE BOOK PROJECT

i. **Uwepo wa Wanafunzi na Programu za Mafunzo**

a. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaosoma Elimu ya Amali wanajumuisha makundi mbalimbali, wakiwemo wenye mahitaji maalumu.

b. Kubainisha fani zinazotolewa na kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya teknolojia.

ii. **Uwepo wa Walimu na Wataalamu wa Elimu ya Amali**

a. Kuwajengea uwezo walimu waliopo kupitia mafunzo ya mara kwa mara.

b. Kushirikiana na sekta binafsi na vyuo vya ufundi ili kupata wataalamu wa muda mfupi wa kufundisha kozi maalumu.

c. Kuwahamasisha walimu wa Elimu ya Amali kupokea mafunzo ya kisasa yanayolenga mabadiliko ya teknolojia na soko la ajira.

iii. **Wasimamizi Elekezi wa Karakana na Maabara**

MZUMBE BOOK PROJECT

a. Kuhakikisha kuwa wasimamizi wa karakana na maabara ni wataalamu wenye ujuzi wa fani husika.

b. Kuweka utaratibu wa usimamizi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo.

iv. **Mikakati ya Kuboresha Elimu ya Amali**

a. Kubainisha na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji maalumu katika Elimu ya Amali.

b. Kupanua ushirikiano kati ya shule na taasisi zinazojishughulisha na masuala ya amali.

c. Kushirikiana na jamii ili kuhakikisha Elimu ya Amali inapata msaada wa rasilimali na uhamasishaji.

d. Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali toshelevu kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Amali.

e. Kuweka mikakati ya uhamasishaji wa Elimu ya Amali kwa walimu, wazazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla.

MZUMBE BOOK PROJECT

v. **Miundombinu ya Mafunzo ya Amali**

a. Kujenga na kuboresha karakana, maabara, maktaba, madarasa, na mashamba darasa kulingana na fani zinazotolewa.

b. Kuhakikisha kuwa vifaa vya kufundishia vinapatikana kwa viwango vya kutosha na kwa ubora unaohitajika.

vi. **Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

a. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Amali ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu hiyo.

b. Kuhakikisha kuwa walimu na wanafunzi wanapatiwa mafunzo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa kujifunza kwa njia za kidijitali.

vii. **Ushirikiano na Sekta ya Uzalishaji na Biashara**

a. Kupanua ushirikiano kati ya shule, vyuo vya amali, na sekta ya uzalishaji ili kuwezesha wanafunzi kupata mafunzo kwa vitendo.

MZUMBE BOOK PROJECT

b. Kuweka utaratibu wa programu za mafunzo kazini kwa wanafunzi kwa kushirikiana na sekta ya viwanda na huduma.

c. Kuhakikisha kuwa sekta binafsi inashiriki katika kuboresha mitaala ya Elimu ya Amali ili iwe na manufaa kwa soko la ajira.

viii. **Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji**

a. Kuweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi katika Elimu ya Amali.

b. Kuhakikisha kuwa kuna upimaji endelevu wa ufanisi wa Elimu ya Amali kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

c. Kushirikisha sekta ya ajira katika tathmini ya programu za Elimu ya Amali ili kuhakikisha kuwa wahitimu wanakidhi vigezo vya soko la kazi.

ix. **Usimamizi na Uratibu wa Elimu ya Amali**

a. Kuimarisha usimamizi wa programu za Elimu ya Amali katika ngazi zote za elimu ya sekondari.

MZUMBE BOOK PROJECT

b. Kuweka mwongozo wa usimamizi wa rasilimali zinazotumika katika Elimu ya Amali ili kuongeza ufanisi wake.

c. Kuhakikisha kuwa sera na miongozo yote inatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Elimu ya Amali nchini.

**2.2 Maelekezo ya Utekelezaji wa Elimu ya Amali**

Ili kuhakikisha utekelezaji wa Elimu ya Amali unafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia miongozo ya sera, taasisi zote zinazohusika na utoaji wa elimu hii zinapaswa kutekeleza yafuatayo:

i. **Kutekeleza mafunzo ya amali kwa kuzingatia Muundo wa Masomo kwa:**

a. Kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi aliyesajiliwa katika Shule ya Amali au yenye Mkondo wa Elimu ya Amali anasoma masomo sita (6) ya lazima: Business Studies (Elimu ya Biashara), Historia ya Tanzania na Maadili, English (Kiingereza), Mathematics

MZUMBE BOOK PROJECT

(Hisabati), Computer Applications, na Life Skills (Stadi za Maisha).

b. Kusimamia usajili wa wanafunzi katika fani mbalimbali kulingana na matakwa, uwezo, na malengo yao ya baadaye.

c. Kutekeleza ufundishaji wa fani kuu (15) zilizoainishwa, ambazo ni:

1. Uhandisi Umeme (Electrical Engineering);
2. Uhandisi Mitambo (Mechanical Engineering);
3. Uhandisi Ujenzi (Civil Engineering);
4. Uhandisi Magari (Automotive Engineering);
5. Huduma za Usafirishaji (Transport and Logistics);
6. Ushoni (Clothing and Textile);
7. Kilimo, Ufugaji na Usindikaji Vyakula (Agriculture and Food Processing);
8. Ukarimu na Utalii (Hospitality and Tourism);
9. Huduma Saidizi za Biashara (Commercial and Business Support Services);
10. Uchapishaji (Printing);

MZUMBE BOOK PROJECT

11. Uchimbaji na Uchenjuaji Madini (Minerals Extraction and Processing);
12. Urembo na Ususi (Cosmetology);
13. Sanaa Bunifu (Creative Arts);
14. Elektroniki na Kompyuta (Electronics and Computer); na
15. Michezo (Sports).

d. Kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anachagua na kusomea fani moja kuu pamoja na masomo yake wezeshi kwa mujibu wa Kiambatisho A.

**ii. Wamiliki/Wasimamizi wa Shule: Kuhakikisha Uwepo wa Walimu na Mafunzo Endelevu kwa:**

a) Kuajiri na kupanga walimu wenye sifa stahiki kwa ajili ya kufundisha Elimu ya Amali.

b) Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa walimu ili kuwezesha kutumia mbinu za kisasa zinazohusiana na sekta za uzalishaji na maendeleo ya kiteknolojia.

MZUMBE BOOK PROJECT

c) Kushirikiana na taasisi za ufundi na sekta binafsi ili kupata wataalamu wa muda mfupi wanaoweza kufundisha kozi maalumu.

iii. **Wamiliki/Wasimamizi wa Shule: Kuhakikisha Miundombinu na Vifaa vya Kujifunzia Vinapatikana kwa:**

a) Kujenga na kuboresha karakana, maabara, maktaba, madarasa, na mashamba darasa yanayokidhi mahitaji ya fani za amali.

b) Kuweka vifaa vya kisasa vya kujifunzia ili kuhakikisha mafunzo ya vitendo yanafanyika kwa ufanisi.

c) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa Elimu ya Amali ili kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa kwa njia shirikishi.

MZUMBE BOOK PROJECT

iv. **Shule, Sekta Binafsi na Mashirika ya Kisekta: Kuhakikisha Ushirikiano na Sekta ya Uzalishaji kwa:**

a) Kuunganisha shule na taasisi za sekta ya uzalishaji ili kuwapatia wanafunzi fursa za mafunzo kwa vitendo.

b) Kuweka utaratibu wa mafunzo nyanjani kwa wanafunzi kwa kushirikiana na viwanda, taasisi za biashara, na mashirika mbalimbali.

c) Kuweka mifumo ya ushirikiano kati ya shule, sekta ya uzalishaji, na jamii ili kuhakikisha Elimu ya Amali inazingatia mahitaji halisi ya soko la ajira.

v. **Kuimarisha Mikakati ya Kuendeleza Elimu ya Amali**

a) Kubainisha na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa maalumu katika fani za amali.

b) Kufanya uhamasishaji kwa wazazi, wanafunzi, na jamii ili kuongeza ushiriki katika Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

c) Kuhakikisha kuna upatikanaji wa rasilimali za kutosha kwa ajili ya kufanikisha utoaji wa Elimu ya Amali.

vi. **Wizara za kisekta, wadau na Wakuu wa Shule: Kutekeleza Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji**

a) Kutekeleza mifumo ya tathmini ili kupima maendeleo ya wanafunzi na ufanisi wa Elimu ya Amali.

b) Kushirikisha sekta ya ajira katika tathmini ya mitaala na programu za Elimu ya Amali ili kuhakikisha zinaendana na mahitaji ya soko la ajira.

c) Kufuatilia maendeleo ya wahitimu wa Elimu ya Amali ili kubaini mchango wao kwenye jamii na sekta za uzalishaji.

MZUMBE BOOK PROJECT

# 3.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU

## 3.1 Utangulizi

Utekelezaji wa Elimu ya Amali unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali, wakiwemo Serikali, sekta binafsi, jamii, mashirika ya maendeleo, vyombo vya habari, na taasisi za elimu. Ili kuhakikisha Elimu ya Amali inatekelezwa kwa ufanisi na inaendana na mabadiliko ya soko la ajira, kila mdau ana jukumu muhimu la kutimiza.

## 3.2 Wajibu na Majukumu ya Wadau

Majukumu ya wadau mbalimbali yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa kuhakikisha inatekelezwa kwa kuzingatia sera, miongozo, sheria, na mahitaji ya soko la ajira kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uzalishaji, viwanda, kilimo, ujasiriamali, na biashara.

MZUMBE BOOK PROJECT

ii) Kuanzisha mifumo rasmi ya Elimu ya Amali yenye mwelekeo wa mafunzo ya vitendo kwa kushirikiana na taasisi kama VETA na vyuo vya elimu ya ufundi, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata mafunzo ya kisasa kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia.

iii) Kupanua ushirikiano kati ya shule za sekondari na sekta binafsi ili kutoa fursa za mafunzo katika mazingira halisi ya kazi.

iv) Kuhakikisha uwepo wa walimu wenye ujuzi wa kutosha katika fani mbalimbali za amali kwa kushirikiana na taasisi za elimu kama ADEM, vyuo vya ualimu, vyuo vikuu, na kuendeleza mafunzo endelevu kwa walimu ili kuwezesha kufundisha kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia na mbinu za kisasa.

v) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika Elimu ya Amali, kwa mfano, kwa kutoa vivutio vya kodi kwa makampuni yanayochangia vifaa vya kufundishia au kushiriki katika ufundishaji wa Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

vi) Kushirikiana na sekta binafsi na mashirika ya maendeleo ili kupata rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Elimu ya Amali, kupitia miradi ya ufadhili kama wa Benki ya Dunia, UNESCO, na washirika wengine wa maendeleo.

vii) Kuimarisha usimamizi na tathmini ya Elimu ya Amali kwa kutumia mifumo ya kidijitali ya ufuatiliaji, ili kubaini changamoto za utekelezaji na kufanya maboresho ya mara kwa mara kwa kushirikiana na NECTA, NACTVET, VETA, na taasisi nyingine za elimu.

viii) Kuhamasisha na kuratibu upatikanaji wa miundombinu ya Elimu ya Amali, ikiwa ni pamoja na karakana, maabara, mashamba darasa, na vifaa vya kisasa vya mafunzo ili kuwezesha ujifunzaji wa vitendo kwa wanafunzi.

ix) Kuanzisha na kusimamia kanzidata ya kitaifa ya miradi ya Elimu ya Amali, kwa lengo la kuratibu utekelezaji wake kwa ufanisi na kuhakikisha miradi ya amali inapangwa kwa uwiano sahihi kulingana na mahitaji ya maeneo husika.

MZUMBE BOOK PROJECT

x) Kusimamia mfumo wa utoaji wa vyeti kwa wahitimu wa Elimu ya Amali, kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), NACTVET na taasisi nyingine za tathmini ili kuhakikisha vyeti vinatambulika rasmi katika soko la ajira na vyuo vya elimu ya juu.

### 3.2.2 Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI)

i) Kuratibu uanzishwaji wa vituo vya Elimu ya Amali katika kila halmashauri kwa kushirikiana na WyEST ili kuongeza fursa za mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi.

ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya miundombinu na vifaa vya kufundishia Elimu ya Amali, ikiwemo ujenzi wa karakana, maabara, na mashamba darasa.

iii) Kuratibu upatikanaji wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha Elimu ya Amali katika shule za sekondari kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na taasisi za mafunzo ya ualimu.

MZUMBE BOOK PROJECT

iv) Kuandaa mfumo wa tathmini ya utekelezaji wa Elimu ya Amali katika ngazi ya halmashauri kwa kushirikiana na WyEST na NECTA ili kufuatilia ubora wa elimu inayotolewa.

v) Kuratibu utekelezaji wa Elimu ya Amali katika ngazi ya mikoa, halmashauri, kata na shule kwa kuhakikisha rasilimali, walimu, na vifaa vinapatikana kwa wakati.

vi) Kuhakikisha mipango ya maendeleo ya halmashauri inajumuisha Elimu ya Amali ili kusaidia kufanikisha utekelezaji wake.

vii) Kuratibu uhusiano kati ya shule, jamii, sekta binafsi, na taasisi za mafunzo ya amali ili kuwezesha utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa vitendo.

viii) Kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika kuchangia vifaa na miundombinu ya Elimu ya Amali kama karakana, maabara, na mashamba darasa.

ix) Kuripoti maendeleo ya Elimu ya Amali kwa WyEST na wadau wengine kwa kutumia mifumo rasmi ya taarifa na ufuatiliaji.

MZUMBE BOOK PROJECT

### 3.3 Ngazi ya Mkoa

i) Kuhakikisha Elimu ya Amali inajumuishwa katika mpango wa maendeleo wa mkoa ili kuwezesha utekelezaji wake kwa ufanisi.

ii) Kuratibu usimamizi wa utoaji wa Elimu ya Amali katika halmashauri zote za mkoa kwa kuhakikisha rasilimali zinapatikana na zinasimamiwa ipasavyo.

iii) Kusimamia utekelezaji wa miongozo na sera za Elimu ya Amali ndani ya mkoa kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na WyEST.

iv) Kuhamasisha wadau wa ndani ya mkoa kushiriki katika utoaji wa Elimu ya Amali, ikiwemo mashirika ya sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali.

v) Kuandaa taarifa ya maendeleo ya Elimu ya Amali na kuiwasilisha OR-TAMISEMI na WyEST kwa ajili ya tathmini na maboresho.

MZUMBE BOOK PROJECT

### 3.4 Ngazi ya Halmashauri

i) Kuhakikisha shule zote katika halmashauri zinatekeleza Elimu ya Amali kulingana na sera na miongozo ya kitaifa.

ii) Kuratibu upatikanaji wa walimu wa Elimu ya Amali kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na WyEST.

iii) Kuhakikisha rasilimali kama vifaa vya ufundishaji na miundombinu vinapatikana ili kuwezesha utoaji bora wa Elimu ya Amali.

iv) Kuandaa mipango ya mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Amali kwa kushirikiana na NECTA, VETA, NACTVET, na taasisi nyingine za mafunzo ya ualimu.

v) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa Elimu ya Amali kwa kutoa fursa za mafunzo katika maeneo halisi ya kazi kwa wanafunzi.

vi) Kuratibu ukusanyaji wa takwimu za Elimu ya Amali na kuzitumia kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wake.

MZUMBE BOOK PROJECT

### 3.5 Ngazi ya Shule

i) Kutoa elimu kuhusu fani za amali kwa watahiniwa wakati wa uchaguzi wa kuingia ngazi ya elimu inayofuata;

ii) Kuratibu shughuli za uatamizi kwa wanafunzi wanaosoma Elimu ya Amali;

iii) Kutambua mahitaji ya wanafunzi na kuwaelekeza katika fani zinazowafaa kulingana na uwezo wao na mwelekeo wa soko la ajira;

iv) Kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya:

   a) Ubainishaji na uendelezaji wa wanafunzi wenye vipawa na vipaji;
   b) Ushirikiano kati ya shule, jamii na taasisi zinazojishughulisha na masuala ya Elimu ya Amali;
   c) Upatikanaji wa rasilimali toshelevu kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Amali; na
   d) Uhamasishaji kuhusu utoaji wa Elimu ya Amali.

v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wazazi/walezi kuhusu utoaji wa Elimu ya Amali kwa wanafunzi;

MZUMBE BOOK PROJECT

vi) Kushirikiana na wataalamu kutoa mafunzo na ushauri kuhusu utoaji wa Elimu ya Amali shuleni; na

vii) Kusimamia ujazwaji wa taarifa za *selform* kwa wanafunzi kulingana na uwezo, matakwa na malengo ya mwanafunzi husika katika maisha yake ya baadaye.

**f) Ngazi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji**

i) Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Mtaa/Kijiji unaojumuisha mkakati wa kuboresha Elimu ya Amali katika shule na vyuo vya eneo husika;

ii) Kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ya:

a) Kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji kwa kuweka programu maalumu za malezi ya vipaji.

b) Kukuza ushirikiano kati ya shule, jamii, Taasisi za Elimu ya Amali, na sekta binafsi ili kuhakikisha mafunzo yanaendana na mahitaji ya soko la ajira.



MZUMBE BOOK PROJECT

c) Kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Amali, ikiwemo vifaa vya mafunzo ya vitendo.

d) Kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa Elimu ya Amali kwa kupitia mikutano ya kijamii, vyombo vya habari vya mtaa, na programu za uhamasishaji.

iii) Kusimamia utekelezaji wa utoaji wa Elimu ya Amali shuleni na vyuoni kwa kuhakikisha kuwa sheria ndogo ndogo zinazohusu utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali zinatungwa, kutekelezwa, na kusimamiwa ipasavyo;

iv) Kushirikiana na wataalamu wa sekta mbalimbali ili kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kuhusu utoaji wa Elimu ya Amali katika jamii ya mtaa/kijiji;

v) Kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika utoaji wa Elimu ya Amali kwa kuchangia rasilimali za kifedha, vifaa vya kufundishia, na kushiriki katika shughuli za mafunzo kwa vitendo; na

MZUMBE BOOK PROJECT

vi) Kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu ya Amali, kama vile karakana, na maabara za mafunzo ya vitendo, ili kuboresha mazingira ya kujifunza kwa wanafunzi wa Elimu ya Amali.

**g) Wazazi/Walezi na Jamii**

i) Kushirikiana na walimu kubainisha uwezo, matakwa na malengo ya wanafunzi kwa ajili ya maisha yao ya baadaye;

ii) Kuhamasisha watoto wao kushiriki kikamilifu katika masomo ya Elimu ya Amali kwa kuelewa umuhimu wake katika maendeleo yao ya baadaye.

iii) Kushiriki katika vikao vya wazazi na kamati za shule kwa ajili ya kupanga na kutathmini maendeleo ya Elimu ya Amali.

iv) Kutoa mchango wa kifedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Elimu ya Amali shuleni.

MZUMBE BOOK PROJECT

v) Kushirikiana na walimu na shule katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao katika Elimu ya Amali.

**i) Wizara nyingine za Kisekta Zinazotekeleza Masuala ya Amali**

Wizara za Kisekta zinazojihusisha na utoaji wa Elimu ya Amali ni: Wizara ya Fedha; Wizara ya Nishati; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Sheria na Katiba; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Afya; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu; Wizara ya Madini; Wizara ya Ujenzi pamoja na Taasisi zake. Majukumu ya Wizara hizi yatatekelezwa kwa kushirikiana na WyEST na OR – TAMISEMI katika:

MZUMBE BOOK PROJECT

i) Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya Elimu ya Amali.
ii) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipawa na vipaji.

iii) Kuimarisha ushirikiano kati ya shule, jamii, na taasisi za Elimu ya Amali.

iv) Kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kutosha kwa ajili ya Elimu ya Amali.

v) Kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa Elimu ya Amali.

vi) Kushiriki katika utoaji wa mafunzo, usimamizi, na tathmini ya Elimu ya Amali kulingana na maeneo yao ya utaalamu.

**j) Wadau wa Elimu na Wabia wa Maendeleo**

i) Kuchangia juhudi za Serikali katika kuwezesha ujenzi wa miundombinu na vifaa kwa ajili ya mafunzo ya Elimu ya Amali;

ii) Kubuni na kuwezesha utekelezaji wa mipango na miradi ya utoaji wa Elimu ya Amali;

MZUMBE BOOK PROJECT

iii) Kushiriki katika ufuatiliaji, usimamizi elekezi na tathmini ya utekelezaji wa utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali;

iv) Kushiriki katika mijadala ya Kisekta kuhusiana na utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali;

v) Kushiriki katika utoaji wa Elimu ya Amali kwa walimu na wataalamu wa kujitolea; na

vi) Kushiriki katika kutoa mafunzo ya uwezeshaji na utaalamu kwa watekelezaji na wasimamizi wa masuala ya utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali.

**k) Sekta Binafsi**

Sekta binafsi inahitajika kushiriki kikamilifu katika utoaji wa Elimu ya Amali kwa:

i) Kuhamasisha jamii kushiriki katika mipango ya Elimu ya Amali.

ii) Kutoa ushauri wa kitaalamu na elimu.

iii) Kugharamia mafunzo kazini kwa walimu wa Elimu ya Amali.

iv) Kushiriki katika ujenzi wa miundombinu shuleni.

MZUMBE BOOK PROJECT

v) Kushiriki katika utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali.

**l) Taasisi za Kitafiti**

Taasisi za kitafiti zinajukumu la:

i) Kufanya tafiti zinazohusu Elimu ya Amali.
ii) Kutoa matokeo ya tafiti kwa lengo la kuboresha Elimu ya Amali.

**m) Vyombo vya Habari**

Vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika kuelimisha jamii kuhusu Elimu ya Amali kwa:

i) Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Elimu ya Amali.

ii) Kushiriki katika kampeni za uhamasishaji kuhusu Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

n) **Baraza la Mitihani la Tanzania (National Examinations Council of Tanzania - NECTA)**

i) Kuandaa mitihani, kusimamia, kutahini na kutoa matokeo;

ii) Kutoa vyeti kwa wahitimu wa ngazi ya elimu msingi na sekondari ya juu;

iii) Kufanya ulinganifu wa alama kutoka mabaraza yanayosimamia shule za kimataifa;

iv) Kufanya ulinganifu wa alama kwa wanafunzi waliosoma nje ya nchi;

v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu mitaala kwenye shule zinazotekeleza mafunzo ya Elimu ya Amali;

vi) Kuelimisha wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla kuhusu utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali; na

vii) Kushiriki katika mijadala ya kisekta kuhusu utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

**o) Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)**

TET ina jukumu la:

i) Kuandaa mitaala na vifaa vya Elimu ya Amali kwa kushirikiana na WyEST pamoja na VETA.
ii) Kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu mitaala ya Elimu ya Amali.
iii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mitaala ya Elimu ya Amali.
iv) Kuelimisha jamii kuhusu Elimu ya Amali.

**p) Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (Agency for the Development of Education Management - ADEM)**

i) Kushiriki katika mijadala ya Kisekta kuhusiana na utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Amali; na
ii) Kujenga uwezo kuhusu usimamizi wa masuala ya Elimu ya Amali kwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

MZUMBE BOOK PROJECT

q) **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (The National Council for Technical and Vocation Education and Training - NACTVET)**

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) lina wajibu wa:

i) Kusimamia viwango vya ubora katika utoaji wa Elimu ya Amali.

ii) Kufanya ulinganifu wa matokeo ya mitihani ya Elimu ya Amali.

iii) Kushiriki katika mijadala ya kisekta kuhusu Elimu ya Amali.

iv) Kuelimisha jamii kuhusu mitaala ya Elimu ya Amali.

v) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

### r) Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

***Vocational Education and Training Authority*** *(VETA)*

Mamlaka ya VETA inahusika na:

i) Kusimamia na kuendeleza elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

ii) Kushirikiana na shule za amali katika utoaji wa elimu ya ufundi stadi.

iii) Kusimamia utoaji wa mafunzo ya ufundi kwa wahitimu wa sekondari.

iv) Kuimarisha mahusiano kati ya vyuo vya ufundi na shule za amali.

v) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika vyuo vya ufundi.

vi) Kuelimisha jamii kuhusu Elimu ya Amali.

vii) Kushiriki katika mijadala ya kisekta kuhusu Elimu ya Amali.

MZUMBE BOOK PROJECT

# 4.0 UFUATILIAJI NATATHMINI

Ili kuhakikisha utekelezaji wa Mwongozo wa Elimu ya Amali unatekelezwa kwa ufanisi na matokeo yake yanaendana na malengo yaliyokusudiwa, ni muhimu kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utekelezaji. Ufuatiliaji na tathmini utazingatia vipengele vya ubora wa mitaala, ufanisi wa walimu, upatikanaji wa miundombinu na vifaa vya kujifunzia, ushirikiano wa sekta mbalimbali, na athari za Elimu ya Amali kwa maendeleo ya wanafunzi na jamii.

MZUMBE BOOK PROJECT

## 4.1 Malengo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utaongozwa na malengo yafuatayo:

i) Kuhakikisha utekelezaji wa mitaala ya Elimu ya Amali unafanyika kulingana na mwongozo na mahitaji ya soko la ajira.

ii) Kubaini changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa Elimu ya Amali na kutafuta suluhisho sahihi kwa ushirikiano na wadau husika.

iii) Kufuatilia maendeleo ya wanafunzi wanaosoma Elimu ya Amali, ikiwa ni pamoja na viwango vya ufaulu, maarifa ya vitendo, na uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa.

iv) Kuhakikisha rasilimali zinazotengwa kwa Elimu ya Amali zinatumika kwa ufanisi na zinatosheleza mahitaji ya utoaji wa elimu hiyo.

### 4.2 Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Ngazi Mbalimbali

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini umeganywa kwa ngazi tofauti za utekelezaji ili kuhakikisha uwajibikaji wa wadau wote kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Ngazi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)

i) Kusimamia tathmini ya kitaifa ya Elimu ya Amali kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, VETA, NECTA, na NACTVET.

ii) Kufanya tathmini angalau mara mbili kwa mwaka kwa kutumia viashiria vya utekelezaji wa Elimu ya Amali.

iii) Kuchambua na kuandaa ripoti ya tathmini ya kitaifa ili kuwasilishwa kwa Serikali, wadau wa

MZUMBE BOOK PROJECT

elimu, na wabia wa maendeleo kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Elimu ya Amali.

iv) Kuweka mifumo ya kidijitali ya kufuatilia Elimu ya Amali kwa kutumia kanzidata inayoonyesha maendeleo ya shule, walimu, na wanafunzi waliopo kwenye mfumo wa Elimu ya Amali.

#### 4.2.2 Ngazi ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI)

i) Kuratibu na kusimamia ufuatiliaji wa Elimu ya Amali katika ngazi ya mkoa na halmashauri.

ii) Kutoa mrejesho wa kila robo mwaka kuhusu utekelezaji wa Elimu ya Amali kwa WyEST.

iii) Kuhakikisha kuwa kila halmashauri inaunda mpango wa ndani wa ufuatiliaji wa Elimu ya Amali na inatoa matokeo kwa Maafisa Elimu wa Mkoa na Halmashauri.

iv) Kushirikiana na sekta binafsi na mashirika ya maendeleo katika kuhakikisha kuwa tathmini za Elimu ya Amali zinasaidia kuunganisha elimu na fursa za ajira.

MZUMBE BOOK PROJECT

#### 4.2.3 Ngazi ya Mkoa

i) Kusimamia tathmini ya utekelezaji wa Elimu ya Amali ndani ya mkoa kwa kushirikiana na halmashauri na shule.

ii) Kuwasilisha ripoti za tathmini kwa OR-TAMISEMI kila robo mwaka ili kuboresha mfumo wa utoaji wa Elimu ya Amali.

iii) Kuhakikisha kuwa shule zinapata mwongozo kwa ajili ya kutathmini maendeleo ya Elimu ya Amali na utekelezaji wake unazingatia miongozo ya kitaifa.

#### 4.2.4 Ngazi ya Halmashauri

i) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa utoaji wa Elimu ya Amali katika shule zote zilizopo ndani ya halmashauri.

ii) Kusimamia matumizi ya rasilimali zinazotolewa kwa ajili ya Elimu ya Amali ili kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

iii) Kupitia ripoti za maendeleo ya Elimu ya Amali kutoka kwa shule na kuwasilisha taarifa kwa OR-TAMISEMI kila robo mwaka.

MZUMBE BOOK PROJECT

#### 4.2.5 Ngazi ya Shule

i) Kuhakikisha kuwa walimu wa Elimu ya Amali wanajibika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi katika masomo ya amali kwa kutumia upimaji wa darasani na mitihani ya vitendo.

ii) Menejimenti ya shule inatakiwa kuwasilisha ripoti za maendeleo ya Elimu ya Amali kwa Maafisa Elimu wa Halmashauri kila robo mwaka.

iii) Shule zinapaswa kushirikiana na sekta binafsi na mashirika ya maendeleo kwa ajili ya tathmini ya fursa za mafunzo nyanjanii kwa wanafunzi.

iv) Walimu wa Elimu ya Amali wanapaswa kushiriki katika mafunzo ya mara kwa mara kuhusu mbinu za kisasa za kufundisha na kutathmini Elimu ya Amali.

### 4.3 Viashiria vya Mafanikio ya Elimu ya Amali

Ufuatiliaji na tathmini ya Elimu ya Amali utazingatia viashiria vifuatavyo ili kupima mafanikio ya mfumo wa Elimu ya Amali:

MZUMBE BOOK PROJECT

i) Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na programu za Elimu ya Amali na wanaokamilisha mafunzo yao.

ii) Ufanisi wa walimu wa Elimu ya Amali katika kufundisha kwa vitendo na matumizi ya vifaa vya kujifunzia.

iii) Idadi ya shule zilizo na miundombinu ya kutosha kwa ajili ya Elimu ya Amali, ikiwemo karakana, maabara, na vifaa vya kisasa vya kufundishia.

iv) Asilimia ya wahitimu wa Elimu ya Amali wanaopata ajira au kujiajiri ndani ya mwaka mmoja baada ya kuhitimu.

v) Ushirikiano kati ya shule, sekta binafsi, na taasisi za elimu ya juu katika kutoa fursa za mafunzo kwa vitendo.

vi) Matokeo ya tathmini ya kitaifa ya Elimu ya Amali inayofanywa na WyEST na taasisi zake.

MZUMBE BOOK PROJECT

MAREJELEO

African Union (2015). *Agenda 2063: The Africa We Want.* Addis Ababa: African Union.

Federal Institute for Vocational Education and Training. (2021). *Dual vocational training in Germany*. Bonn: BIBB.

Government of Canada. (2022). *Apprenticeship training and skilled trades in Canada*. Otta: Government of Canada.

JMT. (2023). Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023.Dar es Salaam: WyEST.

Lavonen, J. (2021). How the Finnish compulsory school science curriculum emphasises scientific literacy. Eesti Haridusteaduste Ajakiri.

Lee, Y.-F., & Lee, L.-S. (2022). Status and trends of STEM education in highly competitive countries: Country reports and international comparison. Online Submission.

Li, Y., Wang, K., Xiao, Y., & Froyd, J. E. (2020). Research and trends in STEM education: A systematic review

MZUMBE BOOK PROJECT

of journal publications. International Journal of Stem Education, 7(1), 1–16.

Mammes, I., Fletcher, S., Lang, M., & Münk, D. (2016). Technology Education in Germany. In Technology Education Today. International Perspectives. (pp. 11–38). Waxmann Verlag.

Mammes, I., Schaper, N., & Strobel, J. (2012). Professionalism and the Role of Teacher Beliefs in Technology Teaching in German Primary Schools–An Area of Conflict. Teachers' Pedagogical Beliefs, 91.

Margot, K. C., & Kettler, T. (2019). Teachers' perception of STEM integration and education: A systematic literature review. International Journal of Stem Education, 6, 16. https:// doi. org/ 10.1186/s40594- 018- 0151-2

Ministry of Education, S. a. (2023). *Curriculum for Ordinary Secondary Education Form I - IV* Dar es Salaam: Tanzania Institute of Education.

Pappa, C. I., Georgiou, D., & Pittich, D. (2023). Technology education in primary schools: Addressing teachers' perceptions, perceived barriers, and needs.

MZUMBE BOOK PROJECT

International Journal of Technology and Design Education. https:// doi. org/ 10. 1007/ s10798- 023-09828-8

Rasinen, A., Virtanen, S., Endepohls-Ulpe, M., Ikonen, P., Ebach, J., & Stahl-von Zabern, J. (2009). Technology education for children in primary schools in Finland and Germany: Different school systems, similar problems and how to overcome them. International Journal of Technology and Design Education, 19(4), 367–379. https:// doi. org/ 10. 1007/ s10798- 009- 9097-5

Reinholz, D. L., White, I., & Andrews, T. (2021). Change theory in STEM higher education: A systematic review. International Journal of Stem Education, 8(1), 1–22.

Rossouw, A., Hacker, M., & de Vries, M. J. (2011). Concepts and contexts in engineering and technology education: An international and interdisciplinary Delphi study. International Journal of Technology and Design Education, 21(4), 409–424. https:// doi. org/ 10. 1007/ s10798- 010- 9129-1

Sanders, M. (2009). Technology teacher education in the United States.

MZUMBE BOOK PROJECT

*Essential Topics for Technology Educators, 1001*, 239.

Williams, P. J. (2006). International technology teacher education.McGr-Hill Glencoe.

WyEST. (2023). *Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV.* Dar es Salaam Taasisi ya Elimu Tanzania

MZUMBE BOOK PROJECT

VIAMBATISHO

## Kiambatisho A

**Jedwali Na 1: Fani Kuu za Elimu ya Amali na Masomo yake Wezeshi**

| NA. | FANI KUU | MASOMO WEZESHI |
|---|---|---|
| 1 | Electrical Engineering | 1.1 Electrical installation |
| | | 1.2 Bio-energy installation |
| | | 1.3 Wind power plants installation |
| | | 1.4 Solar power installation |
| 2 | Mechanical Engineering | 2.1 Welding and metal fabrication |
| | | 2.2 Refrigeration and air |
| | | 2.3 Fitter machinist |
| | | 2.4 Fitter mechanics |
| | | 2.5 Ginnery fitting |
| 3 | Civil Engineering | 3.1 Masonry and brick-laying |
| | | 3.2 Civil drafting |
| | | 3.3 Boat building |
| | | 3.4 Carpentry and joinery with metal works |
| | | 3.5 Plumbing and pipe fitting |
| | | 3.6 Painting and sign writing |
| | | 3.7 Steel fixing |
| | | 3.8 Well drilling |
| | | 3.9 Wood carving |

MZUMBE BOOK PROJECT

| NA | FANI KUU | MASOMO WEZESHI |
| --- | --- | --- |
| 4 | Automotive Engineering | 4.1 Motor vehicle mechanics |
| | | 4.2 Auto-electric mechanics |
| | | 4.3 Auto-body repair |
| | | 4.4 Motor-cycle mechanics |
| | | 4.5 Agro-mechanics |
| 5 | Electronics and Computer | 5.1 Computer programming |
| | | 5.2 Graphics design |
| | | 5.3 Electronics Repair |
| | | 5.4 Computer maintenance |
| | | 5.5 Mobile phone repair |
| | | 5.6 Office machines maintenance |
| | | 5.7 Film and TV Production |
| 6 | Transport and Logistics | 6.1 Transport operations |
| | | 6.2 Clearing and forwarding |
| 7 | Clothing and Textile | 7.1 Handloom weaving |
| | | 7.2 Finishing craft |
| | | 7.3 Basic knitting |
| | | 7.4 Designing, sewing and cloth technology |
| | | 7.5 Leather goods and footwear |

MZUMBE BOOK PROJECT

| NA | FANI KUU | MASOMO WEZESHI |
|---|---|---|
| 8 | Agriculture and Food Processing | 8.1 Meat processing and technology |
| | | 8.2 Oil seed processing |
| | | 8.3 Animal health and production |
| | | 8.4 Horticulture production |
| | | 8.5 Field crop production |
| | | 8.6 Wood processing |
| | | 8.7 Bee keeping |
| | | 8.8 Fishing and fish processing |
| | | 8.9 Aquaculture and fish processing |
| | | 8.10 Seeed farming |
| 9 | Hospitality and Tourism | 9.1 Front office operations |
| | | 9.2 House-keeping |
| | | 9.3 Food production |
| | | 9.4 Food beverage services and sales |
| | | 9.5 Tour guide and travel operations |
| 10 | Commercial and Business Support Services | 10.1 Business operation assistance |
| | | 10.2 Secretarial |
| | | 10.3 Insurance |
| | | 10.4 Wholesale and retailing |
| | | 10.5 Geospatial technology |
| 11 | Printing | 11.1 Packaging printing |
| | | 11.2 Screen printing |
| | | 11.3 Binding and print finishing |

MZUMBE BOOK PROJECT

| NA | FANI KUU | MASOMO WEZESHI |
|---|---|---|
| 12 | Extraction and Processing of Minerals | 12.1 Jewelry |
| | | 12.2 Salt extraction |
| | | 12.3 Gemology (Gemstone cutting, polishing and carving) |
| 13 | Cosmetology | 13.1 Hair dressing |
| | | 13.2 Beauty therapy |
| | | 13.3 Fitness and nutrition |
| 14 | Creative Arts | 14.1 Acting |
| | | 14.2 Costume and makeup designs |
| | | 14.3 Ngoma performance |
| | | 14.4 Music and sound technology |
| | | 14.5 Music performance |
| | | 14.6 Carving |
| | | 14.7 Dring and painting |
| | | 14.8 Pottery and ceramic |
| | | 14.9 Textile design and small-scale printing |
| | | 14.10 Art and design |
| 15 | Sports | 15.1 Football performance |
| | | 15.2 Netball performance |
| | | 15.3 Track events |

***Chanzo:*** (WyEST, 2023)

MZUMBE BOOK PROJECT